

**TAARIFA YA UJENZI WA MRADI WA MAJI KATIKA KIJJI CHA
KAGUGU KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU
KITAIFA NDUGU CHARLES FRANCIS KABEHO TAREHE 05/06/2018**

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Ninayo furaha kubwa kukukaribisha pamoja na Msafara wote uliofuatana nao hapa Kagugu eneo la Mradi nasema karibu sana na ujisikie upo nyumbani.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Idara ya Maji Mji wa Mbinga ina miradi miwili inayotekelezwa kwa sasa ambayo ni Mradi wa Maji Maganagana pamoja na huu wa Kagugu.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Uzalishaji wa maji kwenye chanzo cha mradi huu wa Maji kwa siku ni lita 172,800 wakati mahitaji ya maji ni lita 112,320. Hivyo sasa uzalishaji wa maji ni mkubwa kuliko mahitaji. Chanzo cha maji kipo umbali wa kilomita 6.5 kutokea kwenye tenki. Jumla ya urefu wa mradi mzima ni kilomita 18. Kukamilika kwa mradi huu wa maji kutawezesha huduma ya maji kwa kijiji cha Kagugu iwe bora.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Mradi huu unajengwa na Mkandarasi OVANS CONSTRUCTION LTD ya Mbinga kwa gharama ya shilingi 493,059,575.00; kazi ya ujenzi ilianza tarehe 15/03/2018 na itakamilika tarehe 07/06/2018. Mradi utahudumia Wakazi 1650 kwa sasa kati ya 4430 wanaotarajiwa kuongezeka baada ya miaka 20 ijayo.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Mradi wa huu wa Maji Kagugu una tenki lenye ujazo wa lita 50,000. Ili kufikia malengo ya ‘kumtua Mama ndoo kichwani’, mradi huu una jumla ya vituo vya kuchotea maji kumi na saba (17), ambapo vituo kumi na tatu (13) tayari vimeshakamilika kujengwa na vituo vinne (4) vitaongezwa. Mradi huu baada ya kukamilika utakabidhiwa kwenye Jumuiya ya Watumia Maji (COWSO) kwa ajili ya uendeshaji na utoaji wa huduma.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Tunaamini ya kwamba Mafanikio ya Elimu iliyo bora kwa Taifa letu rasilimali Maji ya uhakika kwa ajili ya uendeshaji wa Shughuli mbalimbali zinazohusiana na Elimu, upatikanaji wa maji safi na salama mashuleni na kwenye Taasisi zote za wadau wa Elimu, hivyo tunaunga mkono kauli mbiu inayosema. *“Elimu ni Ufunguo wa Maisha wekeza sasa”*

Ahsante, naomba kuwasilisha.

(Eng. NTELEZU P MASANJA)
**Kny.MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YAMJI
MBINGA**